# حِزْبُ اللهِ

# أَمْ

# حِزْبُ الشَّيْطَانِ؟

# JE,

# (CHAMA CHA HIZBOLLAH LEBANON)

# NI ASKARI WA ALLAAH AU NI ASKARI WA SHETANI?

Mtunzi:

Sheikh Ally Sadiki

Tarjama:

Ghalib Abdullaah

**Je, Chama cha Hizbollah Lebanon ni Askari wa Allaah au ni Askari wa Shetani?**

بسم الله الرحمن الرحيم

## Je, ni Askari wa Allaah au Askari wa Shetani?

Je ni nani Hizbollaah (askari wa Allaah) waliokusudiwa katika kauli ya Allaah Ta'alaa:

﴿أُوْلَٰٓئِكَ حِزۡبُ ٱللَّهِۚ أَلَآ إِنَّ حِزۡبَ ٱللَّهِ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ﴾

**[Hao ndio askari wa Allaah (Hizbollaah), tambua kwamba askari wa Allaah ndio wenye kushinda]**[(1)].

Kundi/Askari wa Allaah ni wale wanaomuamini Allaah na siku ya kiama na wanawapiga vita maadui wa Allaah na Mtume wake -Swala na Salamu zimshukie-, ijapokuwa ni ndugu zao wa karibu.

Amesema Imam Ttwabari -Allaah amrehemu-: maana ya Aya hii:

﴿أَلَآ إِنَّ حِزۡبَ ٱللَّهِ﴾

**[Tambua kwamba jeshi lake na wafuasi wake].**

﴿هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ﴾

**[hao ndio wenye kubakia na wenye kushinda kwa kuyapata yale wanayoyataka (mbele ya Allaah), nao ni wenye kushikamana na Baia ya Allaah (kiapo cha utiifu) hapa duniani, pamoja na kumtii Mola wao Mlezi]**[(2)].

---

[1]- Surat Al-Mujaadila/22.

[2]- Tafsiru Ttwabari (Jz. 22, Uk. 495).

## Ni lipi kundi la Hizbollaah la Lebanon?

Kundi la Kishia la Hizbollaah liliasisiwa huko Lebanon mnamo mwaka 1982m, lakini mwaka 1985m lilijiunga na mambo ya kisiasa.

Chama hiki ni zao la harakati za kundi la Kishia la Amal huko Lebanon, kundi linalo dhaminiwa na Nchi ya Iran, na muasisi wake ni Musa As-Sadr.

Hapo awali liliitwa kwa jina lake la asili ambalo ni: Harakat Amal Sshi'iyyah (harakati za matumaini za Kishia), kisha likaitwa kwa jina la Amal Al-Islaam (tumaini la Uislamu), kwa ajili ya kutaka kupanua wigo wake na ili kujumuisha mataifa yote ya waislamu, kwa sababu kundi la mwanzo (Harakat Amal Sshiiyyah) harakati zake ziliishia kwenye mipaka ya kisiasa kwa Mashia wa Lebanon tu, lakini kundi hili la pili litasimamia kueneza Ushia ndani ya nchi ya Lebanon na ulimwengu wote wa kiislamu, kwa hiyo likawa kundi hili ni sawa na mpiganaji mwenye upinzani aliyebeba matumaini makubwa katika kutetea umma wa kiislamu na kulinda matakatifu yake.

Kutokana na vitendo vya kinyama na uhalifu mbaya ambao ulihusishwa na chama cha Harakat Amal Sshi'iyyah, ilikuwa ni vigumu kwa chama kilichoundwa badala yake Amal al-islaamiyyah kubeba majukumu ya kulinda taifa (la waislamu), na kwa ajili ya kuogopea hilo kiliundwa chama kingine kipya ambacho leo kinajulikana kama Hizbollaah[(3)]. Baada ya kubadilisha jina, na kujaribu kujitakasa katika vyombo vya habari, kwamba wao ni wapiganaji hodari (hali ya kuwa ndio wahalifu wa jana). Vipi watu hawa wataweza kupigana Jihad na kuifungua Miji?!

[3]- Tazama kitabu: [Amal Walmukhayyamaatul Falastwiiniyya] (Uk. 131).

**Je, Chama cha Hizbollah Lebanon ni Askari wa Allaah au ni Askari wa Shetani?**

Hakika huo ni mchakato na tamthilia ambayo hukusudiwa ndani yake kuwalaghai waislamu, hasa watu wa kawaida ambao hawajasoma uislamu wao, hawajasoma historia wala hawafahamu chochote kuhusu itikadi sahihi za kundi la Shia Raafidhwa, watu hao wa kawaida wanawahukumu watu na kutathmini haki na batili kupitia vyombo vya habari kama vile: (Televisheni, Watsap, YouTube n.k.), ambavyo kwa asilimia kubwa vinapotosha wala havimwongozi mtu kwenye elimu sahihi kwa kusimulia matukio ya kihistoria kiuhalisia.

Kwa hiyo chama hiki (Hizbollaah) kimekuja kushika nafasi muhimu na ya hatari zaidi kwa umma wa kiislamu kuliko nafasi ya chama kilichotangulia cha Harakat Amal, ambacho kilikuwa ni chama cha Kishia chenye mrengo wa kisiasa.

## Ni Nani Waasisi Kundi la Kishia la Hizbollaah huko Lebanon?

Ndugu muislamu, fahamu kwamba viongozi wa kundi la Kishia la Amal ndio haohao viongozi wa kundi la Hizbollaah.

Nchi ya Iran imetoa juhudi kubwa katika kuasisiwa kundi la Hizbollaah chini ya uongozi wa (Muhammad Husein Fadhlullaah), ambaye amepewa jina la kubandika (Khomein wa Lebanon), (Swabhi At-Tufeily), (Hasan Nasrullaah), (Ibrahim Al-Amin), (Abbas Al-Muusawiy), (Naim Qasim), (Zuheir Kanji), (Muhammad yuzbak) na (Raaghib Harb).

## Hizbollaah ni Chama cha Iran Ndani ya Nchi ya Lebanon:

Wala hatuvuki mipaka tunaposema: Hizbollaah ni chama cha Wairani huko Lebanon, kwani katika taarifa ya kuanzishwa kwa chama hicho, iliyokuwa na kichwa cha Habari: **[Sisi ni nani na ni upi utambulisho wetu?**. Chama chenyewe kilijitambulisha kwa kusema: **[Sisi ni kizazi cha Hizbollaah ambacho Allaah aliwapa ushindi wale wa mwanzo huko Iran, na ambacho kwa mara nyingine kimeundwa tena kwa ajili ya kupandikiza mbegu ya Dola kuu ya Kiislamu duniani… tunashikamana na amri za uongozi mmoja wenye hekima na uadilifu, unaowakilishwa na**

**Je, Chama cha Hizbollah Lebanon ni Askari wa Allaah au ni Askari wa Shetani?**

**Imam mmoja tu mwenye fiqhi na aliyekusanya masharti yote, kwa sasa tunaungana sote mbele ya Imam mmoja mtukufu Ayatollah Al-Muusawi Khomeini (adumu muda mrefu), mwanzilishi wa mapinduzi ya Kiislamu na mchochezi wa mwamko mtakatifu][(4)].**].

Mmoja wa viongozi wa chama hicho (Ibrahim al Amin) mwaka 1987m, aliwahi kuelezea mtazamo huu: **[Hatusemi kwamba sisi ni sehemu ya Iran, bali sisi ni Iran ndani ya Lebanon na Lebanon katika Iran].** Na pia Hasan Nasrullaah: **[Sisi tunaona nchi ya Iran ndio Dola inayotawala Kiislamu na ndio Dola iliyosimama kuwatetea waarabu na waislamu, na uhusiano wetu sisi na Dola hiyo ni uhusiano wa ushirikiano, na sisi tuna urafiki na ushirikiano pamoja na viongozi wa Dola hiyo, kama zilivyokuwa mamlaka za kidini nchini humo…]**

kwa maneno haya imebainika kwamba kundi la Hizbollaah ni harakati za kishia, zimeundwa ili kueneza mapinduzi ya Khomeini katika ulimwengu wa Kiislamu na kile kinachoitwa Wilaayatul Faqih, wakatumia fursa ya matukio yanayojitokeza katika nchi za kiislamu kama ndio mahali pa kueneza fikra zao, wakatumia kauli mbiu za kuvutia na nembo mbalimbali ili kuteka hisia za Waislamu.

## Je, Hassan Nasrullaah Ni Nani na Lipi kundi la Hizbollaah Ambalo Anajinasibisha Nalo, na Ana Mahusiano Gani na Eneo la Mashia la Amal?

Jina lake ni Hassan Abdul karim Nasrullaah (Khomeini wa Waarabu) aliyezaliwa 21 Augost 1960m, alitangazwa rasmi kuwa kiongozi wa kundi la Amal katika mji wa Al-Bazouriyah katika wilaya ya Sour, akasafiri hadi Najaf huko Iraq mwaka 1976m ili kupata mafunzo ya dini ya Maimamu (wa Kishia), aliteuliwa kuwa afisa wa kisiasa wa kundi la kiharakati la Amal na mjumbe wa ofisi ya Kisiasa mwaka 1982m, kisha hakukaa muda mrefu akajiengua kwenye kundi hilo na kujiunga na kundi la Hizbollah, na akateuliwa kuwa kiongozi huko Beirut mwaka 1985m, kisha mjumbe wa kamati kuu na bodi ya chama mwaka 19987m. Pia alichaguliwa kuwa Katibu mkuu (wa chama cha Hizbollah) kufuatia kuuwawa aliyekuwa

[4]- [http://www.khomainy.com/ark/ho

Katibu mkuu Abbas al-Mousawi mwaka 1992m huku akikamilisha muhula wa mtangulizi wake, kisha akachaguliwa mara mbili mwaka 1993m na 1995m, na bado mpaka sasa amebaki kwenye cheo hicho.

## Chama cha Hizbollah na Wilaayatul Faqiih:

Maana ya Wilaayatul Faqiih ni: Itikadi ya Dini na siasa katika Ushia, Muasisi wa itikadi hiyo ni kiongozi wao Khomeini, na makusudio yake ni kwamba mtu anayestahiki zaidi kuwa kiongozi na raisi wa nchi ni mwanachuoni wa Fiqhi ya Dini (ya Shia), ambaye ametimiza masharti maalumu, na huyo ndiye mwakilishi wa (Mahdi) katika kuongoza umma wa waislamu, (imam) ambaye amekingwa na kutenda dhambi na anayesubiriwa kutoka pangoni (kwa madai yao), kwa hiyo hairuhusiwi kuamrisha au kutenda chochote isipokuwa kwa kurejea kwa kiongozi huyo wa Kidini aliyechaguliwa na watu ili awaongoze kwa niaba ya Imam Mahdi anayengojewa.

Anasema Khomeini mwanzilishi wa fikra na mtazamo huu: **"Wanachuoni wa Fiqhi wa sasa hivi (wa Kishia) ndio hoja kwa watu (wote), kama alivyokuwa Mtume ni hoja juu yao, na yeyote mwenye kukhalifu akaacha kuwatii hao (wanachuoni wa Fiqhi wa Kishia) basi hakika Allaah atamuadhibu kwa sababu ya hilo"**[5].

Na anasema Muhammad Husein Fadhlullaah, mmoja kati ya masheikh wao wanaorejewa (katika fatwa): **"Maoni ya Faqiih ('Al-Waliyyul Faqih' mwanachuoni mkubwa wa Fiqhi ya Kishia) yanampa yeye fursa ya kuhalalisha mambo kwa ile sifa yake ya kuwa ni naibu wa Imam, na Imam ni naibu wa Mtume (s,a,w), kama alivyokuwa Mtume ana haki zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao, vivyo hivyo Imam ana haki zaidi kwa waumini kuliko nafsi zao, na mwanachuoni wa Fiqhi aliye mwadilifu ana haki zaidi kwa waumini kuliko waumini"**[6].

Na Khomein anazingatiwa kuwa ndiye kiongozi wa kiroho na kisiasa katika harakati na kazi zote za (chama cha Hizbollah), (Khomeini) aliteuwa kundi la maafisa wa Iran ili kumjulisha yeye kila mara mienendo ya vuguvugu la Mashia huko Lebanon, pia alitoa maelekezo kwa baraza kuu la ulinzi

---

[5]- Tazama kitabu: [Al-Hukuumat al-Islaamiyyah] chapa ya nne (Uk. 109).

[6]- Tazama kitabu: [Wilaayatul Faqiih] cha Muhammad Husein Fadhlullaah (Uk. 46).

kupokea amri na miongozo yake na kupeleka kwenye chama hicho, bila kusahau kwamba kiongozi mkuu wa chama hicho huteuliwa na Khomeini.

Tovuti maalumu ya nchini Iran ilichapisha Makala adimu ambayo Khomeini (akiwa kama kiongozi wa kidini) alimuandikia Hasan Nasrullah (barua akimteua) kuwa ni naibu wake huko Lebanon katika mambo ya kisheria, na kukusanya zaka pamoja na kuzigawa kwa wanaostahiki.

Na pia tovuti ya Baztab ilitangaza habari iliyotolewa na Amiri Jeshi Mkuu wa zamani wa walinzi wa Mapinduzi (ya Iran) Muhsin Razaei, alisema: **"Mwaka 1981m, Khomeini alimpokea Hasan Nasrullah akiwa kijana wa miaka 21, akifuatana na kundi la viongozi wa Harakati wa chama cha Amal, na hiyo ilikuwa katika Huseiniyyah (kituo cha mafunzo ya Kishia) ya huko Jamaran kaskazini mwa Tehran".**

Katika mkutano huo iliripotiwa kwamba Khomeini alimpa Hasan Nasrullaah ruhusa ya kisheria ya kupokea pesa za Khumus (fungu la moja ya tano), zaka na Kafara, na kuzitumia katika matumizi stahiki kwa vile atakavyoamua yeye, katika kustawisha Dini (ya Shia Raafidhwa), hili halikuwa jambo la kawaida kwa Khomeini ambaye (hapo kabla) alikuwa ni mwangalifu sana wa kutoa Ijaza (ruhusa) kwa maulamaa wa Dini ya Kishia, na hili linaashiria imani yake kubwa kwa Hasan Nasrullaaah[7].

Na baada ya kufariki Khomeini, na kushika madaraka Ally Khamenei, yeye akashika nafasi ya Al-waliyyu al-Faqiih (kiongozi wa Wilaayatul Faqiih) ambaye kundi la Hizbollah humrejea yeye katika mambo ya Dini na siasa.

Baada ya hapo aliwachagua watu wawili sheikh Muhammad Yazbek na Hasan Nasrullah kuwa mawakala wake kisheria huko nchini Lebanon, katika kusimamia masuala ya kifedha na sheria, wanapokea pesa (za sadaka) kwa niaba yake na kuzitumia kwa maslahi ya Mashia, na wao wameruhusiwa kuteua mawakala kwa niaba yao.

---

[7]- Kuhusu risala ya Khomeini kumpa uwakala Hasan Nasrullaah tutaitaja katika risala yetu: **[Je, umafahamu nini kuhusu kundi la Nuswairiyyah?].**

## Je, Chama hiki Kina Matawi katika Ulimwengu wa Kiislamu?

Ndio, kuna matawi ya Hizbollah katika nchi zote za kiarabu na wote wanafanana katika itikadi na mfumo, miongoni mwa matawi hayo ni:

1. Chama cha Hizbollah Bahrain.
2. Chama cha Hizbollah Hijaz.
3. Chama cha Hizbollah Kuweit.
4. Chama cha Hizbollah cha Yemen

Na wamefanya matukio mengi maovu katika nchi hizo, baada ya kupata mafunzo na msada kutoka kwa walinzi wa mapinduzi ya Iran na Hizbollah wa Lebanon. rejea kitabu: [Unafahamu nini kuhusu Hizbollah?] (Uk. 38-69).

## Chama cha Hizbollah Lebanon wameshirikiana na Iran katika kupigana na Iraq (wakati wa Saddam Hussein)

Uthibitisho wa kushirikina kwa chama cha Hizbollah pamoja na Iran katika vita baina ya Iraq na Iran, ulitoka kwa baba mlezi wa Hizbollah Ali Akbar Mohtashemi Poue, Balozi wa zamani wa Iran nchini Syria, Waziri wa zamani wa mambo ya ndani, na Katibu mkuu wa mkutano wa kimataifa wa kuunga mkono mapigano ya raia wa Palestina. Yeye ndiye aliyeitoa Hizbollah mwaka 1982m kutoka kwenye chama cha Amal.

Hakika kiongozi huyo ameweka wazi ushirikiano wa wapiganaji wa Hizbollah namna waliyosimama bega kwa bega na Iran katika vita dhidi ya Iraq. Pia aliwahi kuongea katika Gazeti la (Sharq) la nchini Iran kuhusu Hizbollah na matukio yao ya mwisho huko nchini Syria, akasema: **"Sehemu ya uzoefu ya Hizbollah inatokana na uzoefu uliopatikana katika vita baina ya Iran na Iraq, na sehemu nyingine ni kutokana na mafunzo… Hizbollah ilipata uzoefu wa hali ya juu wa vita wakati wa vita vya Iran na Iraq, kiasi kwamba wafuasi wa Chama hicho walikuwa wakipigana ndani ya safu za majeshi yetu au kwa kujitegemea wao wenyewe"[8].**

[8]- Rejea risala inayoitwa: [Maadha ta'rifu 'an Hizbillaah] (Uk. 58-59).

## Taqiyyah katika Maneno ya Hizbollah:

Hizbollah ni mojawapo ya makundi ya Shia Imaamiyyah ambayo yanatumia sana Taqiyyah katika kuamiliana na Ahlus Sunnah.

Imekuja katika kitabu: [Al-Imaamul Mahdi Wamafhuumul intidhwaar] cha mtunzi wake Kaadhim Al-Misbaah (Uk. 240): **"Mwenye kufanya taqiyyah anapigana jihad… lakini anapigana jihad kwa uangalifu na tahadhari kadri awezavyo, na wala si (maana ya taqiyyah) kujiweka nyuma nyuma na kupuuza kama wanavyodhani Mashia wajinga, na haikuwa taqiyyah isipokuwa ni amali ya siri ambayo inawafanywa Mashia kuwa ni jumuiya au chama cha kisiasa cha upinzani kinachofanya kazi zake kwa siri, bali hiyo (taqiyyah) ni namna ya utendaji kazi kwa ile njia wanayotumia Hizbollah, ima kwa sura ya uwazi na ufinyu ambayo inakwenda sambamba na mazingira ya kisiasa…".** Mpaka akafikia kusema: **"Lakini huenda mzungumzaji akatumia lugha ya kuongopa na kutosema ukweli… ikiwa kuna uwezekano wa jambo hilo kuleta madhara endapo atalibainisha.**

**Ninasema:** Yule ambaye atazingatia maneno ya Mshia huyu ataona kukiri kwake kwamba Hizbollah wanafanya taqiyyah katika maneno yao.

Mara ngapi tulikuwa tunasema: Msiwaamini Hizbollah wala msiamini maneno ya kiongozi wao Hasan Nasrullah, kwa sababu Dini ya Shia Raafidhwa ni Dini ya taqiyyah (kuficha itikadi yao), huenda Mshia akasema maneno dhahiri yake ni kweli kumbe ni muongo, yeye anakusudia maana nyingine, kama alivyokiri hilo sheikh wao Kaadhim Al-Misbaah, au akageuza maneno kama anavyofanya Hasan Nasrullah, wala usishangae kwa hilo, kwa sababu Dini ya Shia Imaamiyyah inaruhusu mtu kusema uwongo kwa lengo la taqiyyah, bali hata kumuapia Allaah kiapo cha uwongo. Imekuja riwaya katika kitabu: [Wasaailu Sshia] kutoka kwa Abu Abdillaah amesema: **"Ikiwa mtu ameapa kwa taqiyyah, hapana madhara yoyote (kwake)…",** hakika amesema kweli Imam Shafi (Allaah amrehemu) pale alipowasifu Shia Raafidhwa kwamba ni waongo akasema: **"Sijaona kundi lolote lenye kusema uongo zaidi kuliko (Shia) Raafidhwa".**

## Je, Chama cha Hizbollah Kinaamini Jihad katika Sabiilillah (njia ya Allahh)?

Je, Hizbollah inatamani kuikomboa ardhi gani ya Waislamu duniani, kama vile Palestina au sehemu miongoni mwa ardhi za Waislamu zilizotekwa?

Haijawahi kushuhudiwa katika historia tangu hapo zamani kwamba Shia Raafidhwa wameshiriki vita (Jihad) yoyote ya Waislamu, wala kuukomboa mji wowote, sababu ni kwamba hakuna Jihad kwa Shia Imaamiyyah mpaka atoke Mahdi wao (wa uwongo) katika (pango la Sardabi huko Iraq), kwa sababu Shia wanaitakidi Ghaiybatil Kubra[9] bali riwaya zao zinasema wazi kwamba: **"Bendera yoyote (ya Jihad) itakayonyanyuliwa kabla ya bendera ya Imam Mahdi basi huyo mwenye kuinynayua ni twaaghuti (shetani)"**[10].

Kwa hiyo hakuna Jihad kwa Mashia mpaka atoke Imam Mahdi, atafanya suluhu baina ya Mayahudi na Manaswara, na atawahukumu kwa sheria ya watu wa Nabii Daud, (sheria ya Kiyahudi), pia ataivunja Al-Ka'ba, atapigana na Ahlus Sunnah kwa sababu wao ni maadui wa Shia, na atamfukua Abubakar na Omar (Allaah awaridhie) kwenye makaburi yao na kuwasulubu na mwishowe kuwachoma moto[11].

Ikiwa hali iko hivi, basi maneno anayotumia kiongozi wa chama cha Hizbollah katika hotuba zake kwenye vyombo vya mawasiliano kama vile televisheni (Tv), na kuthibitisha hamu ya Hizbollah wa Lebanon kuikomboa Masjid Al-Aqsa (huko Palestina) kutoka kwa Wayahudi, mfano: [Ewe Aqsa, tunakuja] au [Kutembea, kuandamana kuelekea Aqsa] ni maneno matupu na madai ya uwongo yasiyo na msingi, na hakuna uwongo wa wazi kuliko kauli ya kiongozi wao Hassan Nasrullaah

[9]- Shia wanaitikadi ya: Al-Ghaybatu Ssughra na Al-Ghaybatul Kubra, wanakusudia kwamba: mwanzo Imamu wao wa 12 Mahdi (wa uwongo) mwanzo alipojificha pangoni aliacha mabalozi maalumu ambao wanapokea maelekezo moja kwa moja kutoka kwake kwenda kwa wafuasi wake (Mashia), na hii ndio Al-Ghaybatu Ssughra, lakini ulifika wakati hakuwa tena na mabalozi, ikawa Mashia wamekosa mawasiliano na Imamu, na hii ndio Al-Ghaybaul Kubra.

[10]- Tazama kitabu: [Al Ghayba] cha An-Nu'maani.

[11]- Tazama kitabu: [Al Ghayba] cha An-Nu'maani.

akiwahutubia Wapalestina katika moja ya mahojiano yake alipoulizwa kuhusu msimamo wake kwa watu wa Palestina, akajibu kwa kusema: [Mkituhitaji, sisi tuko pamoja na nyinyi na inatosha]!.

(Amesema hivyo), kwa sababu miongoni mwa itikadi ya Shia Ithnaasharia ni kwamba hakuna kupigana Jihad mpaka atokee Mahdi wao (aliyejificha pangoni huko Iraq). Je ndugu yangu muislamu unajifunza nini katika hili?!

Kubwa zaidi ya hayo soma riwaya zao kutoka kwa maimamu wao:

Imepokewa kutoka kwa Abu Abdillah amesema: **"Hakuna yeyote miongoni mwetu sisi Ahlul Bayt atakaetoka (kabla ya kuja mtetezi wetu Imam Mahd) kwa ajili ya kutetea haki yetu au kuzuia dhulma isipokuwa litampata yeye balaa na itakuwa kufanya kwake hivyo ni kutuzidshia matatizo sisi na (wafuasi) wetu wa Shia"[12].**

## Je, Kuna Mikataba ya Siri Iliyosainiwa Kati ya Hizbollah na Israel?

Anasema Afisa wa ujasusi wa Israel: **"Uhusiano kati Israel na Shia wa Lebanon sio sharti la kuwepo kwa eneo la usalama tu, ndio maana Israel iliweza kufadhili mambo mengi ya Kishia na kuunda aina ya maelewano pamoja nao ili kuondoa uwepo wa Wapalestina…"[13].**

Na aliyekuwa Katibu mkuu wa Hizbollah Subhi al-Tufayli akasema: **"Hizbollah ni walinzi wa mipaka ya Israel"**. Pia amesema: **"Mwanzoni mwa miaka ya tisini zilianza kuonekana dalili za mabadiliko katika sera ya Iran…, zilionekana kupitia makubaliano ya Julai 1993m, kisha makubaliano ya April 1996m, yaliyotiwa Saini mbele ya waziri wa mambo ya nje wa Iran wa wakati huo, kwa kumpa amani adui wa Kiyahudi huko Palestina…".** kisha akasema: **"Matokeo ya makubaliano ya April ni kwamba upinzani ulibadilika hadi kuwa walinzi wa mipaka, kwa hiyo Israel inafanya ushawishi mkubwa kwa Mashia wa kusini mwa Lebanon kuwafanya kuwa ni walinzi wao dhidi ya anayetaka kuwashambulia Israel kutokea kwenye mipaka yake ya upande wa kaskazini"**.

[12]- Tazama kitabu: [As Sahiifat As Saajadiyya Al-Kaamila] (Uk. 16).
[13]- Tazama: [Swahiifat maariifil Yahuudiyyah] (8/9/1997).

**Je, Chama cha Hizbollah Lebanon ni Askari wa Allaah au ni Askari wa Shetani?**

Na imeripotiwa katika gazeti la (The Jerusalem Post) katika toleo lake la Mei/23/1985m: **"Muungano wa maslahi ya Israel haufai kupuuzwa, ambao umejikita katika dhamira ya pamoja ya kulihifadhi eneo la kusini kwa Lebanon na kulifanya kuwa eneo lisilo na mashambulizi yoyote dhidi ya Israel…"**.

Na Taufiq Al Madiiniy amelihimiza jambo hili kwa kusema: **"Kundi la harakati la Amal (huko Lebanon), kwa upande wake lilijitolea kuwazuia wanachama wa mashirika ya Palestina kujipenyeza katika maeneo ya kusini (mwa Lebanon) ili kutekeleza mashambulizi ya silaha dhidi ya jeshi la Israel na dhidi ya vitongoji vya walowezi wa huko Galilaya….".**

## Kwanini Masunni wengi Wamedanganyika na Kundi la Hizbollah la Lebanon na kuamini uwongo wao?

Miongoni mwa sababu zilizopelekea Ahlus Sunnah kudanganyika na uwongo wa chama cha Hizbollah:

1- Watu wengi katika Masuni hawazijui itikadi za Mshia kama vile: kuamini kwao kwamba Qur'an imepotoshwa, Maimamu wao wana daraja za juu kuliko Manabii wa Allaah, kuwakufurisha kwao Maswahaba wakubwa (Abubakar, Omar, Uthman na wake wa Mtume Swala na salamu zimshukie (Aisha na Hafsa), na kwamba Aisha (Allaah amridhie) aliwahi kufanya uchafu wa zinaa, na pia wanamkufurisha kila muislamu asiyekuwa Shia Ithnaasharia.

2- Kufanyia kazi msingi wa Taqiyya, na mmoja wa masheikh wa Kishia anayeitwa Al-Mufid wakati akielezea maana ya taqiyyah alisema: **"Kuficha ukweli na kuficha Imani ndani yake kwa Mukhaalif (asiyekuwa Shia) na kuacha kushirikiana nao kwenye lile ambalo litaleta madhara katika dini (ya Shia) na dunia yao".**

**Je, Chama cha Hizbollah Lebanon ni Askari wa Allaah au ni Askari wa Shetani?**

Ndugu muislamu, hakika Taqiyya ni nyenzo kubwa wanayoitumia Mashia katika kueneza Ushia wao, na ndio sababu kubwa iliyopelekea Masunni kuzikubali kauli za kiongozi wa kundi la Hizbollah Hassan Nasrullaah katika hotuba zake, wakati anapokariri kwamba yeye (eti) ataikomboa Masjid Al-Aqsa (huko Palestina)

3- Vyombo vya habari, vina nafasi kubwa katika kuripoti matukio na kutoa taswira kwa watu kuhusu Hizbollah, kwanini isiwe hivyo! Hali ya kuwa wao ndio wamiliki wa chanel ya **Al-Manaar** ambayo kazi yake usiku na mchana ni kusifia kundi la Hizbollah na kiongozi wake, mpaka limekuwa kundi hilo mbele za watu ni kundi lenye kupigania Dini ya Allaah (Jihad) na ndio kundi pekee limeundwa ili kuikomboa miji ya Waislamu kutoka kwenye mikono ya Mayahudi!!!.

## Je, Nini Wajibu Wetu Kwa Muungano huu wa Kishia dhidi ya Masunni?

Mbele ya kundi hili la Kishia lenye uadui mkubwa dhidi ya Masunni hasa katika Nchi ya Iraq, Syria, Lebanon na nchi nyingine za Kiislamu, ni muhimu kwetu kusimama pamoja kukabiliana na kundi hili. Pia ni wajibu kwa tawala za nchi za kiislamu kumchukulia hatua kali yeyote anayedhamini kundi hili au kushirikiana nalo ndani ya nchi zao, na lazima kuwepo mikakati maalumu baina ya nchi za kiislamu kuanzia ngazi za juu na kuwaunga mkono Masunni kila mahali duniani ili kukabiliana na juhudi ya Irani kuwasaidia Mashia kwa lengo la kufanakisha malengo ya kundi lao hilo. Pia ni wajibu kwa Maulamaa wa Kiislamu, Masheikh, Walinganizi, na Wanafunzi wa kiwango cha kati, kubainisha itikadi za kundi la Shia Ithnaasharia, ambazo Waislamu wengi hawazijui, na pia kuweka wazi mbinu na mikakati ya kundi la Hizbollah dhidi ya Waislamu.

Baada ya kuelezea ukweli huu na uhalifu unaofanywa na kundi hili, je itafaa kwetu sisi kuwaita kwa jina hili: **HIZBOLLAH?** Je hawa ndio Hizbollah (askari wa Allaah) ambao amewasifu katika Qur'an au ni Hizbo Sshaitwani (askari wa shetani) na wafusi wake ambao amesema Allaah:

﴿أُوْلَٰٓئِكَ حِزۡبُ ٱلشَّيۡطَٰنِۚ أَلَآ إِنَّ حِزۡبَ ٱلشَّيۡطَٰنِ هُمُ ٱلۡخَٰسِرُونَ﴾

**[Hao ndio kundi la shetani. Hakika kundi la shetani ndio lenye kukhasirika]**[14]**.**

Amesema Imam Al Qurtubi (Allaah amrehemu) katika kueleza maana ya Aya hii: ﴿أُوْلَٰٓئِكَ حِزۡبُ ٱلشَّيۡطَٰنِۚ﴾ **"anakusudia askari wa sheatani na wafuasi wake"**.

Na aliposema: ﴿أَلَآ إِنَّ حِزۡبَ ٱلشَّيۡطَٰنِ هُمُ ٱلۡخَٰسِرُونَ﴾ **"Tambueni kwamba askari wa shetani na wafuasi wake ndio wenye kuangamia na wenye kupata khasara katika biashara yao .**

---

[14]- Surat Al Mujaadila/19

## CHANEL ZA KISHIA AMBAZO INAPASA MUISLAMU KUTAHADHARI NAZO:

| | |
|---|---|
| 1- Al-Manar | المنار |
| 2- AlanwarAloula | الأنوار الأولى |
| 3- Almaaref | المعارف |
| 4- 4teen | فورتين |
| 5- Alforat | الفرات |
| 6- Beladi | بلادي |
| 7- Alghadeer | الغدير |
| 8- Alawhad | الأوحد |
| 9- Al Ahad | العهد |
| 10- AlmasarAloula | المسار الأولى |
| 11- Al Kout | الكويت |
| 12- Alalam | العالم |
| 13- Taha | طه |
| 14- Press tv | بريس تي في |
| 15- Al-Etejah | الاتجاه |
| 16- Hudhud (kwa ajili ya Watoto) | هدهد |
| 17- Sahar 1 | سحر 1 |
| 18- Sahar 2 | سحر 2 |
| 19- Hudhud Faris | هدهد فارس |
| 20- Dua chanel | الدعاء |

| | |
|---|---|
| 21- Alwahda tv | الوحدة |
| 22- Almahdi Tv | المهدي |
| 23- Al Sirat Tv | الصراط |
| 24- Ifilm | آي فيلم |
| 25- Alanwar 2 | الأنوار 2 |
| 26- AhluBayt fares | أهل البيت فارس |
| 27- Karbala Tv | قناة كربلاء |
| 28- Thaqalayn Tv | قناة ثقلين |
| 29- Essalam Tv | قناة السلام |
| 30- Anajaftv | قناة النجف |
| 31- Watan Tv | قناة الوطن |
| 32- Alhujjatv | قناة الحجة |
| 33- Alkaethartv | قناة الكوثر |
| 34- Almasar Tv | قناة المسار |
| 35- Nahno channel Tv | قناة نحن الفضائية |
| 36- Imam Hussein Channel Tv2 | قناة الإمام الحسين |
| 37- Lualua Channel Tv | قناة الؤلؤة |
| 38- Alnaeem Channel Tv | قناة النعيم |
| 39- Imam Hussein Channel Tv | قناة الإمام الحسين |
| 40- Mawda Channel Tv | قناة المودة |
| 41- Imam Reda Channel Tv | قناة الإمام الرضا |

| | |
|---|---|
| 42- AlWilayah Channel Tv | قناة الولاية |
| 43- Hadi Channel Tv 1,2,3 | قنوات هادي 3،2،1 |
| 44- Fadak Channel Tv | قناة فدك |
| 45- Albakeea Channel Tv | البقيع |
| 46- Etejah English Channel Tv | قناة الاتجاة |
| 47- Alfaq Channel tv | قناة آفاق |
| 48- Alalam News Channel | قناة العالم الأخبارية |
| 49- Ahlulbayt TV English | قناة أهل البيت الإنجليزية |
| 50- Velayat Channel Tv | قناة ولايت |

Allaah ndiye mwenye kuafikisha

Risala hii imekamilika leo asubuhi ya Jumanne

tarehe 27/6/1445H – 9/January/2024M

Tanga Tanzania.